**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

Simu Na: +255 (026) 2740016
Nukushi: +255 026 2740103
BaruaPepe: ded@makete.go.tz
Tovuti:http:www.maketedc.go.tz
***Unapojibu tafadhali taja;***

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri Wilaya ya Makete,
4 Barabara ya Bomani,
59582 MAKETE, NJOMBE,
**S.L.P 6, MAKETE**

**Kumb. Na.EB.22/124/01/66** **17/04/2023**

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Makete imepokea kibali cha ajira mpya chenye Kumb Na FA.97/228/01/9/ “EMP”/06 cha tarehe 06/Aprili/2023 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ifuatayo: -

### 1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - NAFASI 14

**Sifa za muombaji**

i. Awe na Cheti cha Kuhitimu na kufaulu kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI)

ii. Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada katika moja ya fani zifuatazo; Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU**

i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji

ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji

iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kijiji

iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji

v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu

vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika kijiji na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa Njaa, Umasikini na Kuongeza Uzalishaji mali.

vii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaaluma katika Kijiji

viii. Kusimamia, Kukusanya na Kuhifadhi Kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.

x. Kupokea, Kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za kijiji

xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**MSHAHARA.**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina ngazi ya Mshahara wa TGS B I kwa mwezi.

**2. KATIBU MAHSUSI Daraja III- NAFASI 5**

**1.1 Sifa za Mwombaji**

i. Awe mwenye elimu ya kidato cha nne au sita

ii. Awe na Astashahada (NTA Level 5) ya Mafunzo ya uhazili na kufaulu Mtihani wa hatua ya tatu

iii. Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza Maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

**1.2 KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka mbalimbali.

ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.

iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miradi, wageni, tarehe za kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.

vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**1.3 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B1 kwa mwezi.**

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yeyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

ii. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.

iii. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) namba za simu na anwani sahihi.

iv. Maombi yote ya mwombaji yaambatane na nakala ya Vyeti vya Taaluma, vyeti vya kidato cha (IV au IV), Cheti cha Kuzaliwa na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.

v. Testimonals na “Provisional statement of resuls” hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA**

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyako vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya Uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.

vii. Siku ya Usaili kila mwombaji afike na Vyeti halisi (Original) vya Elimu, Taaluma, Kuzaliwa kuzaliwa na Kitambulisho.

viii. Waombaji waliostaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi ni kosa kisheria na wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.

x. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 08/05/2023 saa 9:30 alasiri.

xi. Maombi yaambatanishwe na nakala ya kitambulisho cha **NIDA**.

xii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anwani ya :-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Makete,
S.L.P 6
**MAKETE**

William M. Makufwe
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
**MAKETE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MAKETE

**Nakala:**

1. Katibu wa Tume,
   Ofisi ya Rais,
   Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
   S.L.P 2320,
   **DODOMA.**

2. Tovuti ya Halmashauri
   www.maketedc.go.tz

3. Meneja Redio Kitulo FM
   97.1 FM

4. Mbao za Matangazo
   Halmashauri ya Wilaya
   **MAKETE**